# HUSIANO WA JAMII NA MCHUNGAJI CHUCK SMITH

# NENO LA LEO

## YALIYOMO

**Mintaarafu……………………………………………..……………….…………......1**
**Jaribio la kweli…………………………………..……….………………….. 1**
**Mambo ya kweli naya kutendwa……………………………..……….…………2**
**Kuelewatofauti……………………………………………………...………….. 3**
**Mpangilio wa amri za mungu…………..............................................……... 3**
**Maadili ya kikristo……………………………………………..…………….3**
**Kujitolea kwa upendo……………………………………………….………...  4**
**Mahitaji yasiyo ya kimungu……………………………………….………….… 4**
**Kukaribiana pamoja…………………………………………………….…..… 5**
**Nguvu za kutii…………………………………………..……………….……... 6**
**Mtoto wakati wa kitambo………………………………….…………….….... 6**
**Ndani ya kristo………………………..…………………………………….. 7**
**Baba na mama……………………………………………………….....…..7**
**Adabu…………………………………........................................…......9**
**Neno ……………………………………………………………………………… 10**
**Mwajiri na mwajiriwa ……………………...…………………………………11**
**Muktasari……………………………….......................................…… 12**
**KUHUSU MWANDISHI.......................................................................................... 12**

## MINTAARAFU

Wengi wetu hutamani kuishi vyema. Hivi basi ni muhimu kutambua maisha ya mwanadamu hutegemea vipande viwili .”Na vyote viwili vinategemeana Mara nyingi hujipata hali yetu ya upande umeenda mrama, Kwa mfano:, Tumekorofishana na rafiki na tunatamani kurekebisha mambo.Tunajiona hatufai, tunaanza kujichambua kwa undani ili tuweze kukata kauli.

Jambo ngumu ni kwamba wakati mwingi sisi hujidanganya kwa sababu tukijaribu kutatua shida moja, mbili, zingine zinatokea . Inaonekana ni ngumu kuwa na uhusiano mwema na kila mtu. Hii ndio maana mambo yanaweza kuwa vyema kazini lakini nyumbani kunazama. Kwa hivyo tunaweka bidii kurekebisha hali yetu ya nyumbani, lakini tunajipata katika hali ya kiwewe kwani mambo pia yanaanza kuporomoka kazini.

Lakini ni sharti kujua kwamba maisha ya mwanadamu ndio yawe imara hayategemei kipengele cha upande lakini kile cha juu. Na hiki ndicho cha husiano mwema na muumba wetu na kinasababisha kile cha upande kuimarika. Yesu alisema (“Mathayo 6:33)
Hitilafu za akili ni kwamba wanasayansi au madaktari wakitaka kutibu shida zako za ubinafsi wao huona dalili za ugonjwa tu.

Ukweli wa mambo ni kwamba lazima uhusiano wako uwe dhabiti na mola.
Kwa biblia tunaona kuwa uhusiano mwema lazima tusihi na tutii amri zilizotengwa na Mungu.
Neno la Mungu linatufunza sheria muhimu zinazoleta amani na upendo ndani ya jamii.
Hili ni somo fupi kutoka kitabu cha Wakolosai tatu na Waefeso sita Vinasisitiza umuhimu wa uhusiano wa jamii na vielelezo. Natumai hiki kitabu kitakuwezesha kuchambua neno la Mungu ambalo hufunza amri zake na ahadi za baraka zake nyingi.

## JARIBIO LA KWELI

Jaribio la kweli la kikristo si kanisani mbali ni nyumbani. Si vile waumini ama watakatifu tunaonekana kanisani, ni hali ni matendo ya ukristo kila siku na mienendo yetu.
Kama hamtaweza kuishi maisha ya ukristo nyumbani basi itakuwa bure kujionyesha mkristo nje. Si ngumu kuiga ukristo wakati tulipo kanisani kwani tunaweza kuimba, kusifu/kuabudu na kujawa na Roho Mtakatifu. Si kwamba hatuko haki lakini tunapaswa kuishi vivyo hivyo nyumbani.

Nafaa kuonyesha maisha ya kikristo kwa wale nilio karibu nao kila siku. Uhusiano wangu na Kristo unafaa kudhuru uhusiano wangu na mke wangu. Na kwa huu uhusiano nilio nao na watoto wangu.

Daktari Parker mchungaji mkuu alikuwa akiongea na kanisa la Chicago.Baada ya siku chache ambazo walikuwa wakibarikiwa kupitia kusoma neno na wakati wa kushuhudia ukafika; mwana mke mmoja alisimama na kusimulia “Na shukuru haya mafunzo vile yamenijenga” na vile nimetambua kuwa Mungu ananipenda. Nashukuru uhusiano nilio nao na Mungu kupitia kwa mwanaye Yesu kristo.

Akaanza kukaa na Dr. Parker akamwambia kidogo tu,"Niambie kwa huu uhusiano mpya na Kristo unakudhuru vipi nyumbani? Je unakufanya kuwa mke mzuri?Je uko mzuri kwa mumewe kwa sababu ya uhusiano wako na Kristo?Kweli umefanyika bibi mzuri nyumbani?

Aliguzwa begani na mchungaji aliyekuwa nyuma yake. Akamnong'onezea usiongee juu ya hivyo vipengele ndugu, huyo ni mke wangu?" Uzoefu wetu wa kikristo lazima uonekane kwenye uhusiano wa nyumbani na pia nje.

Amri za ukristo si rahisi, tunajua ukweli na tunatamani haki lakini tunashindwa na matendo.
Kuunganisha maisha mawili tofauti ili yawe kitu kimoja na zifanye kazi pamoja ni kazi ngumu au ya kujitolea shida lazima ziweko. Ndio maana vitabu kuhusu ndoa zimejaa kwa soko, zinasimulia suluhu za ndoa iliyoimarika wanatamani furaha na amani kwenye uhusiano wao wa nyumbani Hii iko sawa na shida ya uzito wa mwili mbinu tofauti zinatolewa ili kupata jibu
Wakiahidi njia rahisi za mikato kama umbila, kufanya zoezi au kujinyima chakula unaweza kupoteza uzito wa paundi hamsini. Rahisi tuma dola kumi pekee ili upate hii siri.
Kila mara tunatafuta njia fupi za furaha na mafanikio. Kwa kweli mafanikio na uhusiano mwema huitaji kujitolea maana kuunganisha maisha ya watu wawili ni zoezi ngumu.

Paulo alikuwa mwenye hekima aliposema, kwa hayo yote wekeni upendo mbele maana ni dhabiti kwa kuunganisha. Wakolosai 3: 14. Ni kwa upendo wa Mungu ambao unafanya kazi ndani yetu na juhudi zetu kuimarisha upendo tunaweza kufa nikiwa kuishi pamoja na kuwa kitu kimoja kwa furaha.

**MAMBO YA KWELI NAYA KUTENDWA**

Kila mmoja wetu anajitambua kivyake, kuna vile unavyoficha na vile ulimwengu unavyokuona kama kuna tofauti kubwa.kati ya haya maoni basi wewe uko na hitilafu, lakini kama tofauti ni kidogo wewe uko sawa.

Basi wewe ni nani?inaonekana kwamba kila mtu ametambua msemo,
"mke mzuri au mwenye furaha ni heshima kwa mumewe"
Kwa sababu yeye hujihisi ndiye amesababisha furaha ya mkewe.
Ni vizuri kujua vile ulimwengu unavyo kutambua ndio uweze kuchukua jukumu ya maisha yako na nyumba yako. "Si makosa yangu"Mwanzo 3:12
Kila mara tunataka kuwapa wenzetu hitilafu zetu."si makosa yangu"hiwezekani kuwa ni mimi kama angerekebisha kidogo" kama angefuata maagizo ya biblia inayofunza kuhusu ndoa, tungeishi kwa furaha.

Kila mara tunataka wenzetu warekebishe mienendo hali sisi hatujioni.
Ninatambua ni sharti kila mmoja katika ndoa kuchukua jukumu la kuimarisha ndoa bila kukosoa mwenzake

## KUELEWA TOFAUTI.

Biblia inasema mke na mume aliumba yeye(Mwanzo 1:27) Haitaji utafiti wowote kutofautisha mke na mume. Lakini kuna tofauti ambazo ni za muhimu kati ya maumbile ya wote wawili na yanastahili kuzingatiwa ili kuishi pamoja kwa furaha.

Wakati Mungu aliumba Adamu aliona hawezi kuishi peke yake Mwanzo 2:18. Kisha Mungu akaumba mwanamke Awa ili binadamu awe ameimarika. Apate upendo ambao hangepata kwa wanyama. Mungu hakuona msaada wowote kutoka kwa wanyama ndiposa akaumba mwanamke.

Kwa maumbile mwanaume ni kiumbe chenye nguvu na kikubwa na mwanamke ni mdogo na mdhaifu

Kwa hekima sidhani kuna tofauti yoyote kati ya mwanaume na mwanamke. Wako sawa hata mbele ya macho ya Mungu.Wagalatia :3:28. Na vile alituumba na maumbile tofauti kulingana na nguvu na (hisia) ndio maana akaweka amri au sheria zakuzingatiwa ili mke na mme wakitii wataishi kwa furaha na fanaka ambazo Mungu anawatakia.

## MPANGILIO WA AMRI MUNGU

Nakubali kuwa Mungu anakupenda na anampango mzuri wa maisha yako. Ni kweli Mungu hutakia watu wake maisha yenye heri na mafanikio. Kweli Mungu ni baba mwenye upendo kwa watoto wake na anataka waishi kwa furaha. Anahuzunika wakati tuko kwa shida au bila amani. Anatamani tuwe nayo ya kutosha.Yohana 10:10. Ndio basi Mungu ameweka amri fulani katika hekima yake kwa maana anatujua kwa uwezo wetu. Akasema hii ndio njia ya furaha, amani, upendo na utajiri. Shida ni kwamba hatutilii maanani Mungu anataka tuzingatie kulingana na biblia tufanye yale yale tunastahili kufanya, lakini matendo yetu hayaandamani na mafunzo ya biblia. Amri za Mungu zinaleta furaha na mafanikio Daudi alisema, *Zaburi 1:1 – 13.
Musa alimwambia Yoshua achukue sheria za Mungu azizingatie mchana na usiku maana atamfanye mshindi na mshuhuri Yoshua 1:18.

Nikitazama mpangilio wa amri ambazo Mungu ametenga, nahisi kwa roho ni kama siwezi kuzitimiza ili niweze kuishi na furaha na sharti nisitii ndio niwe mwenye furaha. Dunia hii imejaa, watu wenye hofu nyingi. Wanajiona kama maisha inawapita bila chochote kizuri. Hii imesababishwa na kutotii amri za Mungu. Lazima zifuatwe bila mjadala na bila shaka ukizitii utaishi kwa amani na furaha tele duniani.

## MAADILI YA KIKRISTO

Jambo la kwanza tunaona maadili ya kikristo inakubali mke na mume kuwa sawa. Maadili ya ugiriki ama ile ya Roma iko tofauti; bwana ndiye mwenye mamlaka kwa bibi yake.
Maadili ya kikristo yanaeleza jinsi bibi anastahili kuishi na mume wake Pia. haki za

watoto kwa wazazi na wazazi kwa watoto. Vile mfanyikazi anafaa kuishi na tajiri wake na vile tajiri anafaa kuishi na wafanyikazi
Tunafaa kujua kwamba hitilafu ya hizi amri za kiroho na za kimwili zinaleta madhara sawa.
Kwa mfano hauwezi kupanda juu ya paa ya nyumba kisha ukaruka chini utavunjika mfupa au kuumia vibaya vilevile hauwezi kuvunja sheria za ndoa utajuta. Yakini! Neno la Mungu ni haki

## KUJITOLEA NA UPENDO

Wanawake wanastahili kushukuru Yesu Kristo na Ukristo kwa jumla maana kabla ya Ukristo mwanamke alikuwa sawa na mtumwa!
Tulipozuru eneo la Guatemala tuliishiwa na gesi. Marafiki tuliokuwa nao wakatangulia kuenda kununua gesi. Tulibaki tukitazama jinsi Mungu alivyoiumba nchi kwa umashuhuri sana ikawa maridadi. Kisha matawi yakaanza kuvuma kutoka juu ya mlima kuelekea tulikokuwa. Kuangalia kwa makini tuliona wanawake watatu wakiteremka polepole huku wakiwa wamebeba kitita cha kuni kichwani. Walishinda wakipasua kuni hizo mchana kutwa na sasa walikuwa wakielekea makwao wapikie waume zao na jamii yote kwa jumla.

Huko Israeli tuliona mengi, wanawake walikuwa mashambani wakilima na kupalilia na hata kupanda hali waume zao waliketi kitako na kuburudika na kikombe cha kahawa huku wakiuza kondoo. Wanawake hawa wa Guatemala na Israeli hufanya kazi nyingi sana hawana haki au mamlaka. Ukristo umewafanyia wanawake mengi mazuri na yenye manufaa.Barua ya Wakolosai Paulo anaanza na wanawake anasema Wakolosai 3:18, Wanawake wanasema wamechoshwa na mambo ya kunyenyekea waume zao lakini ni muhimu kunyenyekea.
Ni mahali pamoja kwenye biblia ambapo tunaona bibi akiongoza mume katika shamba la eden na kutoka wakati huo tuko taabani.
Amri ya Mungu ni kwamba mume awe kichwa cha nyumba naye mke anyenyekee mumewe.
Mpangilio huu unafaa kuwa Bwana anyenyekee Kristo kama vile Kristo mwenyewe alinyenyekea Mungu. Baba kama bwana atanyenyekea Kristo naye bibi atakuwa amenyenyekea Kristo kupitia kwa mumewe.

## MAHITAJI YASIYO YA KIMUNGU

Sifikiri ni hekima kwa bibi kunyenyekea bwana ambaye mahitaji yake si ya Kristo au kiMungu. Ni ujinga kufuata ukafiri wake na mambo hayaambatani na sheria zisizo za ukristo na hudai kwamba Mungu atakulinda, usikubali kamwe!. Paulo alisema Waefeso 5:22 Pia kwa wakorintho 1 aliweka mpangilio huu kutoka sehemu yoyote basi amri ya Mungu itakuwa imeondoka.
Bwana ni kichwa cha bibiye kama vile Kristo ni kichwa chake(bwana) la si hivyo bibi ni lazima anyenyekee Kristo kwanza. Petro alisema katika Matendo ya mitume 5:29 Lazima tutii Mungu kwanza kuliko binadamu Hata nyumbani kwetu kama kumtii Mungu maana kazi huwa rahisi.

Nilisoma kuhusu bwana mmoja ambaye alikuwa akijiburudisha mvinyo na marafiki zake kwenye kilabu kimoja, walipokuwa wakikaribia kufunga, bwana huyo akacheza kamari nao akawaambia waende kwake wamwamshe bibi yake awatengenezee chakula bila shaka atafanya kwa furaha na huku akitabasamu. Walikubaliana kwani walijua hio ilikuwa mzaha na watashinda hizo pesa. Waliandamana na walipofika walipigwa na butwaa kwani huyu bibi alionekana mwenye furaha wakati wote akitengeneza hicho chakula. Baada ya kula na kumalizana deni zao waliona wamshauri huyu bibi jinsi alivyo vumilia maisha kama haya ya dhuluma. Aliwajibu kuwa yeye ni mkristo na kwa sababu bwana yake si mkristo raha yake ni fupi na anangojea majuto na hukumu hali yeye anangojea kuishi kwa furaha mbinguni milele pamoja na Kristo. Maneno haya yalimkera bwana huyo hadi akaokoka baada ya muda mfupi au siku chache.
Mungu alijua jinsi alivyo muumba mwanaume ndio maana akaamrisha mwanamke anyenyekee mumewe. kwa kawaida mwanaume anapenda kutambulika na kusifiwa. Hakuna kitu humfurahisha kama kuonyeshwa yeye ndiye mwenye mamlaka. Kinacho mfurahisha mara nyingi ni kutambua kwamba yeye ndiye kiongozi na mwerevu.

Kama rafiki yangu Peterson alivyoisimulia jinsi alivyoanza kampuni ya Peterson baby furniture.
Ilikuwa kitambo miaka ya thelathini, walikuwa wakitoka Burbank wakienda maonyesho ya ulimwengu huko San Francisco. Walipokuwa wakiondoka ikawa hakuna nafasi ya kile kiti cha mtoto maana waliandamana na marafiki wengi. Lakini bibi yake alimshauri kuwa yeye ni mwenye hekima nyingi na anaweza kukiunda kiweze kujikunja kisha kutosha ndani ya buti ya gari. Waliporudi alishughulika usiku na mchana hadi alipokiunda. Kila mtu alipokiona hicho kijigari alitamani yake. Na hapo ndipo kampuni ya Peterson baby furniture ilianza. Bwana huyu alijitoa kumfurahisha bibi yake ili asimuone vingine isipokuwa hivyo.

## KUKARIBIANA PAMOJA

Kwa hakika ni lazima kila mmoja kujitolea mhanga asilimia kwenye mambo ya ndoa. Maana ni amri ya Mungu bwana awe kichwa cha familia, naye bibi anyenyekee bwana yake maana ni vyema mbele ya Mungu. Kama hivyo washauri hapo awali maadili ya kiKristo anaonyesha kwamba bwana ampende bibi yake kwa moyo wake wote (Wakolosai 3:19) Naye maadili ya kigiriki si lazima bwana ampende bibi yake anaweza kuoa bibi wa kando na wa halali wa kuzaa watoto! Hili jambo ya upendo ni lazima kujitolea. Kama upendo ambao ulionyeshwa na Mungu wakati alipotoa mwanawe wa pekee aje afe kwa ajili ya dhambi zetu. Hii ndio namna ya upendo ambao bwana anastahili kuonyesha bibi yake kama vile kristo alivyopenda kanisa (Waefeso 5:25) Mungu alipanga haya mambo hivyo maana alijua hisia za mwanamke. Jambo muhimu mwanamke anahitaji kutunzwa kwa mapenzi, hili ni jambo kutokana na maumbile. Ndio maana kila mara anataka kudhibitishiwa kuwa yuko sawa; kama utasikia swali… nywele yangu hii vipi? Hili rinda likoje? Nakaa vipi? Ndiposa bwana anastahili kusema yule sawa mrembo maridadi anang'ara wanaume amkeni!

Wakati mwingine tunajipata sehemu nyingine ya uhusiano wetu. Badala ya bibi kunyenyekea anamua kutotii sheria kukataa mashauri na kukataa maoni ya mume wake. Jambo ambalo linafanya mwanaume kuhisi vibaya. Na vile maelewano hayapo tena uhusiano unazidi kuzama nao wanazidi kutengana bibi anazidi kutotii naye bwana anakasirika. Na sasa mambo haya yakirekebishwa kulinganana na maadili ya kikristo, upendo na furaha zitadumu kwenye jamii bila shaka. Lakini nani atajitolea kwanza, ili ni jambo ngum. Ndio mara nyingi jamii nyingi zinazidi kutengana. Maana bwana atafikiri "nilijaribu kuonyesha upendo akaona mzaha tu". Bibi kwa upande mwingine atafikiri " nilimnyenyekea akadhani mimi ni mjinga". Ndio maana ndoa huvunjika na mnajipata kortini mkitaka talaka.

Shida hii inafaa kutatuliwa na watu wote wawili, mpige magoti na kuomba msamaha mbele ya Mungu kisha kuanza kutii sheria alizotenga. Bibi aombe msamaha kwa kutotii bwana yake naye bwana aombe msamaha kwa kutompenda bibi yake, kama Kristo alivyopenda kanisa. Basi wote wawili wanafaa kuelewana na kushauri Roho Mtakatifu awaongoze.
Bwana " Mungu nisaidie niweze kuonyesha bibi yangu upendo aweze kuihisi amani".
Bibi "Mungu nisaidie nielewe na niache kumkosea mume wangu bali nikubaliane naye mambo yote atakayofanya, hata ingawa ni ya kijinga! Ni kijua ya kwamba tuko pamoja kwa upendo wako na hio ndio tunahitaji, nataka kunyenyekea mume wangu.

## NGUVU ZA KUTII

Uhusiano mwingine kwa mpangilio ni ule wa watoto na wazazi ( Wakolosai. 3:20) Sheria za Mungu, wanastahili kutii wazazi na kuwa na nidhamu njema. Waefeso ( 6:1) Ahadi nyingi za Mungu zinategemea kwa mfano ahadi ya maisha marefu inategemea kama mtoto atatii na kuwaheshimu wazazi wake. Zamani kabla ya Kristo, mtoto asiyetii wazazi alikuwa anapelekwa mbele ya wazee na kushtakiwa kulingana na makosa yake. Hapo wakipatikana na makosa walitupiwa mawe hadi kufa siku zake zikawa chache duniani

## MTOTO WAKATI WA KITAMBO

Wakati Paulo alipokuwa akiandika barua ya Waefeso, Warumi walikuwa hawatambui haki za watoto. Baba alikuwa na mamlaka kwa watoto wake hata kama wako miaka hamsini, yeye ndiye alikuwa na amri ya kumweka hai au kifo. Hata akiamua kumuuza kama mtumwa, alikuwa na haki ya kufanya chochote atakacho nao. Barua ilipatikana ambayo ilikuwa imeandikwa kwa bibi mmoja na mumewe. Alitoa hisia zake kuhusu mtoto aliyekuwa amembeba tumboni. Alimwambia kama ni wa kike amtupe maana hatakuwa wakati wakuzaa. Watoto wengi walitupwa kisha kuokotwa na kufanywa watumwa. Hata kabla ya Roma kuteka nyara Israeli watu waliokuwa wakiishi canaani, kutoa dhabiu ya watoto wachanga haikuwa jambo la kushangaza, hakika wataalamu wamechimba nyumba nyingi na kupata vijichupa vyenye mifupa ya vijitoto. Walifanya hivyo kama ishara ya baraka na bahati kabla ya kujenga nyumba.

Ukristo umeondoa mambo haya mabaya kuhusu mtoto, maana ni lazima kuheshimu uhai

na uwapende. Unaweza kufikiri ni jambo la kawaida kupenda watoto wako lakini kuwa baadhi ya desturi zisizo za kiKristo ambazo mtoto huonekana kama mzigo na ongezeko la shida katika jamii. Wakati huo Paulo alishauri watoto kutii wazazi wao maaana hii ni haki.(Waefeso 6:1). 2Timoteo 3:1-2 Paulo anaonyesha vile wakati wa mwisho watoto watakavyokosa kutii wazazi wao. Pia Warumi 1:30 aonyesha kwamba tabia hizo zilikuwa kama kuoza kwa nidhamu.

## NDANI YA BWANA

Neno linasema watoto watii wazazi wenu. Watii wazazi walio ndani ya Bwana Kristo maana hii ni haki Waefeso 6:11. Kuna baadhi ya wazazi wengi ambao wanataka watoto watii au wakubaliane na desturi zao ambazo siza kiMungu kamwe kama kuomba shetani. Nimeshauri vijana wengi ambao walikuwa wameadhiriwa na baba zao kingono na mateso ya aina nyingi kwangu hii naona kwamba ni jambo la vitisho ambaye binadamu anaweza kufanya mtoto.
Kama mtoto anataka kuenda kanisa na anastahili kufanya kazi ya ziada kwanza.
Nivyema watoto kutii wazazi wao walio ndani ya bwana.
Mimi nilibahatika kupata wazazi waliompenda Mungu.
Nyumba iliyo na furaha ndio nyumba Mungu anatakia watoto wake.
Roho yangu inawaendea watoto vijana wote wa enzi hizi!
Hatutafuti kuwalaumu watu wengine kwa shida zetu.
Maana mvua inyeshapo watu wengine hushukuru na wengine hulaumu hata jua

Wewe ufanye vipi? Maoni yako ni yapi? Lakini naelewa kwa sababu ya mazingira tuliyolelewa lakini ukiwa ndani ya Bwana unaweza kupaa au kujitoa kwenye hali uliyonayo.
Hata kama mama yako alikuwa malaya au baba yako alikuwa mlevi hufai kuishi ukilaumu mazingara ya kale.
Roho mtakatifu atakuongoza, tumeona vijana wengi wakijitoa maana wako ndani ya Bwana. Kwa ajili ya Yesu Kristo vijana wengi wamerudi nyumbani wakiwa viumbe vipya na hivyo inasababisha wazazi kugeuza mawazo kuhusu Ukristo /wokovu. Mungu ameteua jamii nyingi kwa ajili ya vijana kuokoka. Wazazi wameona jinsi yesu kristo anavyobadili watu.

## BABA NA MAMA

Maadili ya ukristo sio tu "watoto watii wazazi wenu"lakini ni "kina baba, msiwadharau watoto wenu wasije wakakosa moyo. Mara nyingi hatuwatii watoto wetu moyo. Ninaamini ya kuwa mtoto anatolewa moyo kwa kunyimwa mambo mengi. Tunaweza kuweka vikwazo vingi katika njia zao. Mtoto anapokua unapaswa kuifanya nyumba yako isiweze kuharibiwa na mtoto. Ikiwa una vifaa ambavyo haungependa vichezewe au viharibiwe, viweke mbali na mtoto badala ya karibu naye. Kwa njia hii, hautapata jukumu la kusema "hapana, hapana" kila wakati aelekeapo kwa vifaa vyako. Inafaa kuwe na vidhibiti visivyo na haja vinaweza kumtoa mtoto moyo na kumpatia mwelekeo mbaya wa kuanzia maisha. Nimewaona watoto wadogo wakitembea nyumbani wakisema "hapana, hapana, hapana, hapana". Ninaamini kuwa mtoto anaweza kutolewa moyo na

kutohisi na serikali ya umiliki. Si lazima tuseme “Fanya kwa sababu nimesema ufanye! “Wazazi wanastahili kuwa wazi na kuelewana na watoto wao.

Nimefikiri ya kuwa mtoto anaweza kutolewa moyo na mzazi ambaye ana ungumu wa kupendezwa. Siku nyingine ufuoni pwani, mwanamke alikuja na familia yake na kutandika blanketi mchangani. Alisema, “usitapakaze mchanga kwenye chakula! Kuwa mwangalifu!usiende kwenye maji! Tuko hapa kujichangamsha na tutajichangamsha!”Wakati huo, umechanganyikiwa sana uko tayari kwenda nyumbani. Pia, kuna haja ya kuepuka ile tabia ya kupata makosa katika kila kitu ambacho mtoto anafanya. Kwa mfano, anakuonyesha picha ambayo alipaka rangi halafu unasema, “mbona ulipitisha kwenye mstari hapa?” Tamshi hili laweza kumvunja moyo mtoto. Watoto wanastahili kutiwa moyo. Kama wazazi, inatupasa kuwa waangalifu. Mara nyingi, hatupendezwi kwa urahisi. Tunaweza kumvunja moyo mtoto kwa kushikilia kutopendezwa kwetu kwa muda mrefu. Ni maoni yangu kuwa mtoto anapoomba msamaha, ni jukumu letu kumsamehe. Usiendelee siku nyingi ukisema, “siamini ulifanya hivyo!siamini! “-ukishikilia makosa yake siku baada ya siku. “Sahani yangu ghali imevunjika!”
Ingekua aje kama Mungu angetufanyi hivyo?Tukikosa na kumwomba Mungu msamaha, hatutaki awe na ungumu kutusamehe na kutoisahau dhambi yetu kwa siku nyingi. Ni fikra yangu kuwa mtoto anaweza kutolewa moyo kwa kuelekezewa madai ya haraka ambayo ni ya uongo.
Nilikuwa na baba mwema, lakini hakuwa bila makosa. Na nilikua na ndugu mdogo, Bill ambaye alikua mkorofi sana. Kabla Bill kuzaliwa, babangu alimwambia mamangu, “ukijifungua mtoto mkorofi, nitakununulia gari. “sijui yaliyotendeka, lakini alipata mtoto mkorofi. Ndugu yangu bill alikua kijana, mvulana katika kila ncha ya mwili wake, na babangu alimsifu na kumpenda sana. Bill alizaliwa baada yetu, hivyo basi tulimfanya na kumbeba mtoto na kumharibu. Kila wakati Bill alipoanza kulia, babangu alikua karibu kupoteza akili. Bill alijua haya. Kwa hivyo kila mara ndugu yangu mwingine na mimi tulifanya chochote kisichomfurahisha, angesema, “Nitakushika! “- na hapo angeanza kulia. Babangu angekuja akikimbia, huku akiutoa mshipi wake na kutucharaza sisi vijana wazee. Halafu angeuliza,. “kuna shida gani hapa? “Kila wakati ndugu yetu Bill angeanza kulia, tungekimbia kwa sababu babangu angetucharaza kwanza kabla ya kuuliza maswali. Si wakati wote nilikuwa bila makosa, lakini nilipata kichapo mara nyingi hata ingawa sikuwa nimehusika. Hiyo ilikuwa hali ya babangu. Alitekeleza kichapo kwanza, halafu akauliza maswali baadaye. Kama tutaelekeza kidole cha lawama kila wakati kwa madai ya uongo na kuwa na haraka ya kufikia hukumu. Jambo ambalo huwavunja moyo sana.
Ninaamini kuwa mtoto huvunjwa moyo wakati kila mara anaonywa kutokana na hatari “Hapana! Huendi nje kucheza mpira! Unaweza ukaumia. Unaweza kujikwaa kidole. Mpira ukikugonga kidole vibaya unaweza kuumia………. Ni vyema kama hatutaendesha baiskeli yako. Ni hatari kuiendesha.” Basi, kuishi ni hatari. Kumkanya mtoto kila mara kwa sababu ya hatari inaweza kukumvunja moyo.

Sasa, kama mzazi, unapaswa kuonyesha tahadhari, hekima na hukumu. Ninaamini kuwa watoto wanapaswa kutahadharishwa dhidi ya hatari fulani kama kuingia kwa gari la mtu wasiyemjua. Lakini hakuna njia ya kumwangalia siku nzima na kumchunga

kutokana na kuumia. Hii ni hali ya kuwa na maendeleo maishani. Ninaamini kuwa mtoto anaweza kuvunjwa moyo kwa kumpa mtihani wa maadili ya utu ambayo hayaitajika katika umri wake mdogo. Kwa mfano, mtoto wa miaka miwili akipandwa na mori. Haustahili kusema, " Ah, una roho mbaya!" Nimesikia kuhusu kijana mdogo ambaye kifua chake kilipigwa picha na kijana akaanza kulia kwa sababu alikua mweusi katika picha. Ninafikiri kuwa kumhukumu mtoto kwa sababu asiyoelewa kunamvunja moyo. Ni fikra yangu kuwa tunawavunja moyo watoto nyakati zingine kwa kuwakataza kuelewa maswala ya Mungu hata ingawa wanavitaka. Tunasema, "U mchanga bado. Hauelewi." Yesu alisema, "Yeyote ambaye hataupokea ufalme wa Bwana Mungu kama mtoto mdogo, hataingia ufalme wa mbinguni. (Mariko 10:15). Kwa mfano, tunaweza kumwambia mtoto wa miaka sita au saba aliyekaa katika huduma ya kushiriki mwili wa Bwana Yesu kanisani na anataka, "Hapana, hawezi kushiriki. U mdogo bado". Lakini rohoni, anampenda Yesu. Labda haelewi marupurupu yake (sijui kama nayaelewa), lakini ni maoni yangu kuwa watoto wanafaa kururhusiwa kushughulika na mambo ya kiroho. Nitayakumbuka matamshi ya Yesu, "Waache watoto wanijie, usiwanyime." Ni maoni yangu kuwa wanapaswa kutiwa moyo na kuruhusiwa kujihusisha na maswala ya kiroho. "Kina baba, msiwaelekeze watoto wenu katika njia ya laana, bali waelekeze katika mapenzi na njia za Bwana Mungu. (Waefeso 6:4). Mojawapo ya shida kubwa ambayo nimeona kwa wazazi ni ile tabia ya kumchezea mtoto hadi akachoshwa. Nimewaona wazazi na watoto wao wadogo – mzazi anamnyoshe kama kumpa mtoto chupa, halafu kurudisha piridi mtoto anapotaka kuchukua huku akicheka na kumnyoshe tena. Mtoto anachanganikiwa kwa kitendo hiki asijue la kufanya na mzazi anapata kicheko na ridhisho kuona mtoto ameghadhabika. Hilo ni mojawapo ya vitendo vya ukatili ambayo mzazi anaweza kufanya.

Wafunzeni watoto katika heshima na tabia za Bwana Mungu. Solomoni alisema, " Mlee mtoto katika njia anazopaswa kufuata: na atakapozeeka, hataziacha."Methali.22:6). Ni jukumu letu kama wazazi kuchukua wakati kuwafunza, watoto wetu katika tabia na heshima ya bwana Mungu.

## ADABU

Kwa kawaida ya jinsi yetu, sisi ni wenye dhambi. Daudi alisema, "Wanapotea wakati tu wanapozaliwa, huku walisema uongo." (Methali 58:3). Alitambua ile hali ya kukosa ya mtu wake. Kuna maana ya undani katika ile hali ya kuruhusu, au uhuni wa kufanya jambo. "Wache watende wanavyotaka. Usinikatae. Waache wajielezee kwa uhuru." Naonelea kuwa Dakitari Spock kwa matamshi na maandishi haya ameikosea nchi yetu. Mtoto aliyeachwa kuwa katika hali yake ya kawaida ya utu si vizuri bali ni dhambi na laana. Maandiko yanasema, "Ujinga umeshikamana na roho ya mtoto, kiboko cha kurekebisha tabia kitatoa na kuweka. Mbali na yeye". (Methali. 22:15).

Neno "adabu" linaashiria maana ya kurekebisha tabia kwa kuadhibu. Ni wajibu mgumu kufunza watoto wako. Unachukua wakati. Ni rahisi kuwaacha wafanye badala ya kuwakangua. Lakini maandiko yasema, "Mtoto aliyeachwa kujitunza humwaimbisha mama yake" (Methali. 29:15). Ni muhimu sana katika kurekebisha tabia ya watoto wetu kuwa isiwaepuke katika mioyo yao kuwa tunawapenda, na kuwa wako salama katika upendo huo na kuwa wakionyesha tabia njema, hawatakuwa na shaka ya upendo huo. Kila mtoto kwa kawaida hushungulika maswala ya kindani. Na kila anapopokea kichapo,

unasema, “Unanichukia! Hakuna anipendaye tena! Hunipendi! “Hatupendi kusikia madai kama haya. Lakini Bibilia imeandikwa, “Mwenyezi Mungu huwakosoa awapendao.” Kitabu cha methali kinasema, “Asiyetumia fimbo yake kumkosoa kijana wake, anamchukia. Wakati mwingine, tunahairisha ama tunachukua wakati kutekeleza adhabu. Kwa kufanya hivyo, tunawaumiza na kuwadhuru watoto, kwani, anapojua amekosa, njia moja nzuri ya kuisaidia nafsi yake kutokana na hali ya kukosa ni kutekeleza adhabu. Watoto wengi wana shida za akili. Wanaifungia mioyo mwao ile hadi ya kuishi wamekosa ambayo haijashugulikiwa na wazazi wao.

Nilipokuwa mdogo na kumkosea baba yangu kwa kutomtii, angesema, “sawa mwanangu. Ukifika nyumbani, nenda katika chumba chako. Nitakuja kuongea nawe. “Nilifahamu hasa alivyoamanisha. Alitamka maneno yake kwa kutumia mshipi. Lakini nilijua nimekosa. Hatukuongeleshana na baba yangu tulipokuwa tukielekea nyumbani. Singeweza kumwongelesha. Nilikuwa nimekosa. Angekuja chumbani mwangu na kusema, “Mbona ulifanya hivyo.” “Sijui baba, nilifanya tu”. “Mwanangu, nilikwambia usifanye hivyo. Lakini hata hivyo, bado ulifanya. Kwa nini?” “Sijui!” Lakini ukweli ulikuwa kwamba nilijua. Nilifanya hivyo kwa kutaka, lakini sikutaka kumwambia hivyo. “Sawa mwanangu. Itanibidi kukucharaza kwa matendo yako.” Basi ningecharazwa. Nililia, kwani nilitambua kuwa nilipolia kwa nguvu, singepata kichapo kingi. Nililia mfano wa mtu anayekaribia kufa. Baadaye angetoka na moyo mzito, na nilibaki nimelala huku nikitamani kufa. Ningekuwa maiti basi angejihurumia kwa kunicharaza! Lakini baada ya muda, mama angeniita kwa chakula cha jioni. Ningekimbia katika chumba cha maamkuli. “Habari yako, baba!” mambo yalikuwa sawa sasa. Sikuwa mwenye makosa tena. Ukuta ulikuwa umeporomoka sasa. Nilikuwa nimeadhibiwa, hivyo, sikuwa na kosa tena. Hilo lilikuwa jambo la kale ambalo halikunisumbua moyoni na kichwani tena. Hakukuwa na jambo mbaya, hata hivyo, kama kukosa na kutogunduliwa. Ningekaa mezani lakini nisimwangalie baba. Hakujua nimekosa, lakini niliogopa asigundue. Kosa langu lilisumbua roho yangu sana, na baada ya siku mbili au tatu hivi, nafsi yangu ilikuwa imedhoofika kwani furaha kuu na kuinua moyo wangu wakati tunashungulikia na kusuluhisha makosa yetu!.

## NENO.

Kama wazazi, inatupasa kutahadhari tusije tukawaadhibu watoto wetu tukiwa na ghadhabu, kwa sababu kuna uwezekano wa kumwadhibu vikali. Wazazi wengi wanakosa wanapotishia kumwadhibu mtoto wao. Usiwahi kutishia kuadhibu. Ahidi kumwadhibu na usivunje ahadi yako. Wazazi wengine wanatishia watoto wao kila wakati. “Nitakugonga kichwa chako ukifanya hivyo tena.!” Hatufanyi hivyo, kwa hivyo, usitamke matamshi hayo. Unamtishia mtoto kila wakati hadi akaacha kushungulika tena. Ni vitisho tu-na anajua. Mtoto wako akijua kuwa neno lako ni la kweli, haitakubidi kumpazia sauti. Utakacho takiwa kufanya ni kungojea tu. Kupaza sauti ni ishara ya unyonge. Ni ishara ya kushindwa tu. Ni ishara ya kushindwa kumtia adabu. Hunibidi kumpazia sauti mbwa wangu kwa sababu nilishindwa tu. Lakini nikisema, NYAMAZA, SHERMAN!” ananyamaza. Kwa nini? Kwa sababu mimi ni mvivu. Mimi ni mvivu sana kumtia adabu.

Mara nyingi, tabia hii ni kweli kwa watoto wetu. Hatujajifunza kuwaadabisha na neno. Tumechukua tabia mbaya ya kupaza sauti. Paulo alimwandikia Timotheo, "Kutoka utotoni, umeyajua maandiko matakatifu" (2 Timotheo 3:15). Timotheo alikuwa amefunzwa na kuadabishwa katika neno la Mungu. Baraka zilizoje!.

Watoto kwa kawaida hawataelekea kutenda mema. Ni lazima uwafunze umuhimu wa uzuri, ulimi wa kweli na utu, usimfunze uongo. Watachukua tabia hii peke yao kwa kawaida..

Itakubidi umfunze kutodanganya. Atafanya hivyo peke yake. Itakubidi umfunze kusema ukweli. Kuna ile hali ya nafsi zao kuelekea katika njia za uovu, hivyo basi, inabidi wafunzwe na kutiwa adabu.

Ni lazima watoto wafunzwe katika njia na heshima ya Mungu. Lakini utakapofanya hivyo, utapitia nyakati za majaribio katika kipidi fulani maishani mwao. Wataacha kuamini wazazi wao na kuamini wanayotaka. Utapitia shida kiasi watakapokuwa wakijaribu mabaya yao, lakini daima utakuwa na amani kuwa watarejea kwa yale uliyowafundisha utotoni. Kwa hivyo, usishituke. Kuwa na amani kwa Mungu atawarejesha kwake kama ulikuwa mwaminifu katika mafunzo yako na utatuzwa na wokovu wao.

## WAAJIRI NA WAAJIRIWA

Mwisho, Bibilia inagusia kuhusu "watumwa na watumishi" na kuweka masharti fulani ya kufuatwa. Siku hizi, hakuna watumwa na watumishi, bali waajiri. Lakini ni maoni yangu kuwa masharti ya "Mtumwa" yanalingana na ya "Mwajiriwa". "Tii kwa kila jambo watumishi wenu katika mwili, sio kumfurahisha mwanadamu, lakini kwa umoja na moyo, ukimwinua Mungu" (Wakolosai. 3:22). Ninaamini kuwa unafaa kuwa mwajiriwa mwema katika kazi yako kama shahidi wa Yesu Kristo. Ninaamini ni vyema ukiwa msema kweli. Si vizuri kutumia wakati wako ukizuru ama kushuhudia kazini. Unafaa kuipatia kazi yako juhudi jasho lako.

Unaweza na unafaa kushuhudia wakati wa mapumziko na chakula cha mchana. Lakini sio ushuhuda mzuri kwa mwajiri wako kama wakati wote utashuhudia mwajiriwa-mwenzake anapotakiwa kuwa kazini. Mwajiri wako anakuangalia tu na anakuona ukimsumbua mwenzako akifanya kazi yake. Huo ni ushuhuda mbaya wa Yesu Kristo. Ni sawa na kumwibia mwajiri wako. Ninahisi kuwa mwajiriwa afaaye kabisa na azaaye matunda mengi kama shahidi wa Yesu. Sio kufanya na kijicho, ama kama kumfanyia binadamu, lakini kama kwamba unamfanyia Bwana "Chochote ufanyacho, fanya na moyo wako wote, kama kwamba unamtendea Bwana Mungu, sio binadamu. Ukiwafahamu kuwa utapokea kwa Bwana tuzo la kweli" (Wakolosai. 3:23,24).

Waanjiri msiwanyime watumwa wenu haki yao sawa, mkifahamu kuwa nanyi mna Mkubwa mbinguni. (Wakolosai. 4:1). Bibilia imemtendea vyema mfanyi-kazi. Mungu huwa katika upande wa mfanyi-kazi. Anaongea dhidi ya mishahara isiyo ya haki zaidi ya mara moja. Mungu Anasema, "Nendeni sasa, enyi matajiri, lieni kwa pambazuko la shida zenu zitakazowajia." Matajiri wameiba na kuwanyima mishahara na marupurupu, sasa adhabu yenu iko tayari(Yakobo 5:1-4). Mungu anaongea dhidi ya kunyimwa mshaara na marupurupu sawa. Ninaamini kuwa mwajiri ana wajibu wa kuwapatia waajiriwa wake mishahara na marupurupu sawa, lakini waajiriwa wanapaswa kuifanyia kazi. "Ukikumbuka kuwa wewe pia una mtumishi mbinguni." Ni muhimu ukumbuke kila

wakati kuwa kuna Hakimu mwishoni ambaye atahukumu wote. Huyu ni Bwana Mungu.

## MUKTASARI.

Tumepitia kwa ufupi uhusiano wa binadamu zinazoambatana na nafasi fulani katika jamii ambazo nimepitia. Kama mwajiri, kama baba, kama bwana, kama bibi, kama mama, kama mtoto, ama kama mwajiriwa. Nafasi yangu kulingana na maandiko ni ipi? Ninaweza kuitekelezaje nafasi yangu?.

Mungu nisaidie. Kwani natambua kuwa nina wajibu kwa Mungu kama mtumwa wake, nina wajibu kwenu kama familia ya Bwana katika nafasi aliyonitwika kama mchungaji wa wanakondoo, na ninatambua wajibu wangu kwa bibi na watoto wangu na ninajaribu kuambatanisha na kutekeleza matakwa yote na shida zinazohusika – hakuna njia ya kuyatekeleza!.
Kama Paulo alivyosema, “Nani atoshaye kwa mambo haya?” (2Wakorintho. 2:16). Lakini Paulo anasema ninamshukuru Mungu kwa, kutosheleka kwetu si kwetu, bali ni kwa Kristo. Tunafunzwa kumgeukia kwa msaada, Mwelekeo na nguvu katika kila jambo.

## KUHUSU MWANDISHI.

CHUCK SMITH, Mtumishi wa Bwana Yesu Kristo, amekuwa mwalimu wa Bibilia zaidi ya miaka ishirini na tano. Ni mchungaji wa Calvary Chapel wa Cost Mesa, California – huduma kubwa ukufunzi na uchungaji. Mafunzo na matamshi yake ya Bibilia yamewasaidia sana maelfu ya wasikilizaji wa radio na wasomi. “Neno la leo” huduma ya utangazaji ya kikristo hueneza vitabu, vijitabu vya ujumbe na video duniani kote.

JINSI YA KUWEKA JAMII YAKO PAMOJA.TUKAJIFUNDISHE MAADILI YA BABA,MAMA, KIJANA NA MSICHANA.

UHUSIANO WA JAMII UNAONYESHA MIPANGILIO YA KUWEKA MAPENZI YA KIFAMILIA IKIWA HAI.
Kujua na kutii neno la Mungu huleta amani, furaha na raha.

Na mchungaji Chuck Smith.